BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kwanza – Tarehe 27 Aprili, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 05 Machi, 2022.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2022/2023.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

1. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

   Wananchi wengi wemekuwa wakiulalamikia utaratibu wa watu waliopotelewa na simu zao kutakiwa kutoa fedha vituo vya Polisi, ili kupewa barua ya kupeleka katika Kampuni ya simu. Aidha wananchi hao wanapofika katika kampuni hiyo, hutoleshwa tena shilingi elfu tano na kampuni ili kupewa laini mpya, bila ya kupewa risiti yoyote.

   Kwa kuwa Serikali imekuwa inasisitiza malipo yote yawe na risiti Je, Serikali inachukuwa hatua gani kwa Jeshi la Polisi na kampuni za simu ambazo hazitoi risiti wakati wa huduma hiyo.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

17. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

   Mabadiliko ya tabia nchi yanaendelea kuathiri mazingira ya nchi yetu kwa kuharibu hadi maeneo ya makaazi ya wananchi.

   (a) Je, Mheshimiwa Waziri ni lini ulitembelea maeneo ya makaazi ya wananchi katika kijiji cha Bubujiko, Gawani, Chasasa, Mkwajuni na Sebuwatu vilivyo katika jimbo la Wete na kuona uharibifu mkubwa uliosababishwa na mabadiliko ya tabia ya nchi.

   (b) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuyanusuru makaazi hayo yasiendelee kuharibika ili wananchi waendelee kuishi kwa amani.

   (c) Je, Wizara yako inawaambia nini wakaazi wa maeneo hayo katika kuwahakikishia usalama wa mali zao.

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

61. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Serikali kupitia Ofisi ya Rais imeanzisha kitengo maalum cha Sema na Rais Mwinyi (SNRMWINYI), kitengo ambacho kimewajengea matumaini mema wananchi waliowengi kwa vile wanaweza kuwasilisha kero zao mbali mbali kupitia kitengo husika na kujibiwa. Hata hivyo, gharama ya mfumo na mafanikio yake hayajawekwa bayana.

(a) Je, ni zipi gharama za awali za uendeshaji wa mfumo huo wa SNRMWINYI.

(b) Je, hadi sasa kuna malalamiko mangapi yamepokelewa na mangapi kati ya hayo yameshapatiwa ufumbuzi.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

13. MHESHIMIWA ZAINA ABDALLA SALUM (Nafasi za Wanawake) Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa utaratibu iliojipangia wa kutoa leseni, kufuatia malipo ya uchukuaji taka kwa wafanyabiashara wetu.

(a) Kwa kuwa leseni hukatwa mwaka hadi mwaka. Je, kuna utafiti gani uliofanyika na kupelekea malipo ya uchukuwaji taka yalipwe kupitia leseni.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kinacholipwa kupitia leseni ya mfanyabishara.

(c) Je, malipo ya taka kupitia malipo ya leseni, ni utaratibu wa kisheria.

## Wizara ya Afya:

41. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuendelea na ujenzi wa hospitali sambamba na uboreshaji wa vituo vya afya, kwa lengo la kuimarisha huduma ya afya kwa wananchi wake.

(a) Ni kiasi gani Wizara inalizingatia suala la uwepo wa hospitali maalum kwa ajili ya "Physiotherapy"

(b) Kwa kuwa uhitaji wa huduma ya "Physiotherapy" ni muhimu kwani kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya (kiharusi) je, Wizara itazingatiaje angalau kila Wialaya kupatikana huduma hii.

(c) Je, Wizara ina wataalamu wangapi wanaoshughulikia "Physiotherapy".

72. MHESHIMIWA ABDALLA ABAS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Katika shehia ya Nungwi kulikuwepo kituo cha afya ambacho kilitoa huduma kwa wananchi wa Nungwi na vijiji jirani, lakini kwa sasa huduma hizo zimehamishwa na kupelekwa katika Kijiji cha Maafa.

(a) Je, kwa sasa kituo hicho kinafanyiwa shughuli gani.

(b) Je, ni lini Serikali itarudisha huduma ya afya katika kituo cha awali, ili kuwaondoshea shida wananchi waliopo katika maeneo hayo.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukiimarisha kituo hicho na kuzirejesha huduma zake za awali.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

8. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.:

Kwa miaka mingi barabara inayotoka Gongoni – Kisima Majongoo na kuunganisha Kiswandui – Kikwajuni "Wireless" imekuwa katika hali mbaya. Aidha, ahadi kadhaa zimetolewa katika vipindi tofauti ya kutengenezwa barabara ile inayounganisha pia barabara kuu za Michenzani – Mnazi

Mmoja – Darajani.

(a) Je, ni lini Wizara itaitengeneza barabara ile ili kuondoa kero ya muda mrefu sana ya wananchi wa maeneo hayo.

(b) Ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo ipo muda mrefu, kwa nini haitekelezwi.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

19. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejitahidi sana katika ujenzi wa madarasa mapya, pia yapo madarasa ambayo yamejengwa na wananchi ambayo hayajamalizika katika baadhi ya skuli za msingi na sekondari Unguja na Pemba.

(a) Je, Wizara inayo taarifa ya skuli hizo ambazo wananchi wamejitolea na hadi sasa hazimalizika.

(b) Je, ni lini Serikali itaendeleza ujenzi huo ikiwa ni pamoja na kuyaezeka kwa lengo la kuondoa kabisa tatizo la nafasi kwa wanafunzi wetu.

49. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kitengo cha mitihani ni kitengo muhimu na nyeti sana kwa maendeleo ya elimu katika nchi. Na kwa kuwa Baraza la Mitihani la Zanzibar hadi leo hii halina jengo lake maalum wala kiwanda mahsusi cha kuchapishia mitihani yake.

(a) Je, ni lini Serikali italipatia Baraza la Mitihani la Zanzibar (BMZ) jengo lake maalum la Ofisi.

(b) Je, ni lini Serikali italipatia Baraza hili kiwanda chake mahsusi cha kuchapishia mitihani kwa lengo la kuondoa uwezekano wa udanganyifu wa mitihani.

## Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

22. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na malalamiko mengi ya wakulima wa karafuu ambao mashamba yao yamekodishwa na Serikali, kufuatia agizo la Serikali la wakulima hao kurejeshewa fedha zao.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea mpaka leo wakulima hao kutopatiwa malipo yao.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
27 Aprili, 2022. KATIBU WA BARAZA